



## BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

### ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

#### **BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

#### **MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 08 Juni, 2024**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua zitasomwa.

#### I. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

##### **Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2024/2025.

##### **Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa Mwaka 2024/2025.

#### II. **MASWALI:**

##### **Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

248. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)  
– Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la uharibifu wa mazingira licha ya mikakati na jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali.

Je, Sheria inayohusiana na uhifadhi na utunzaji wa mazingira

haihitaji marekebisho yoyote kwa sasa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

23. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali kuja na mpango wa ujenzi wa skuli za kisasa zinazoendana na wakati wa karne hii, ikiwa ni pamoja na skuli ya Chukwani. Mnamo tarehe 06/04/2023 viongozi wa jimbo na baadhi ya wananchi wa Chukwani walishuhudia makabidhiano ya hati ya kuanza ujenzi wa skuli hiyo na kuahidiwa kuwa ikifika tarehe 15/12/2023 skuli hiyo itakuwa imeshakamilika kila kitu na kukabidhiwa. Hata hivyo, kitu hicho hakijafanyika hadi leo hii huku wananchi wa jimbo la Kiembesamaki hawajui kinachoendelea.

- (a) Ni kwa nini makabidhiano hayo hayajatimia mpaka sasa.
- (b) Kutokana na uchakavu mkubwa na hatarishi sana wa jengo linalotumika sasa, je, ni hatua gani za dharura Wizara yako imezichukua kunusuru maafa yasitokee.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

150. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hivi karibuni, Serikali imejenga miradi mikubwa ya maji pamoja na miundo mbinu yake ili kuondoa tatizo la maji kwa wananchi wa Zanzibar.

- (a) Je, ni kwa kiasi gani miradi hii imeteklezwa.
- (b) Je, kwa kiasi gani dhana mzima iliyokusudiwa ya huduma ya maji safi na salama imewafikia walengwa.
- (c) Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi kuhusiana na kupatikana huduma ya maji safi na salama kwa sasa.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

70. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwa kuwa vyombo vingi vya mwani vya mita tano vimetolewa kwa wananchi.

- (a) Je, ni lini Wizara itawapatia wavuvi waliopo Pemba vyombo vya uvuvi.
- (b) Je, ni lini wavuvi hao watapatiwa nyavu za kuvulia kwa bei nafuu.

**Wizara ya Afya:**

15. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na hospitali ya Chukwani kutoa huduma za afya kwa muda wa masaa ishirini na nne (24), hali ya hospitali hiyo hairidhishi ingawa Serikali kuitia Wizara ya Afya iliyahi kuifanyia ukarabati mkubwa kwa lengo la kuboresha huduma ya afya kwa wananchi, ukarabati ambao bado haujakamilika huku hospitali hiyo ikiendelea kukabiliwa na uhaba wa baadhi ya vitendea kazi na ukosefu wa dawa.

Je, ni upi mkakati wa Serikali kumaliza changamoto hiyo katika hospitali ya Chukwani.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar,  
08 Juni, 2024.

  
(Raya Issa Msellel)  
**KATIBU WA BARAZA**